Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu

ni neema ya Uzima



Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Jambo ambalo walitaka kuwaficha!

Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu

ni neema ya Uzima

Safari ya nafsi yangu yaelekea wapi?

(Kitabu hiki kinapatikana katika lugha ya kifaransa na ya kiingereza)

First Edition in Swahili: April 2022
1ère édition en Swahili: Avril 2022

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Was Ihnen verschwiegen werden sollte:
Reinkarnation
Die Gnadengabe des Lebens

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait autorité

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Kuamini kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili wa mwanadamu kulianza tangu mwanzo wa dunia. Zaidi ya nusu ya idadi ya wanadamu duniani huchukuwa kanuni ya sababu na matokeo yake na imani kwamba mwanadamu anaweza kuzaliwa upya mara nyingi duniani kama ukweli asilia. Imani hiyo imo ndani ya tamaduni zote, si katika tamaduni ya mashariki tu, kama vile dini ya kibudha na ile ya kihindu.

Katika nyakati za awali za Ukristo asilia, maandishi mengi yaliyokuwa yanachukua tendo la kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili mpya kama ukweli dhahiri yalikuwa yanasambazwa na watu, kwa mfano «Pistis Sophia», mojawapo ya Injili apokrifa (injili zilizofichwa). Kitabuni humo, Yesu alisema kuhusu kurudi kwa nafsi toka ahera na kuingia katika mwili mpya wa mwanadamu, kwamba «imekunywa kikombe cha usahaulifu».

Maandishi hayo, na mengine mengi, haikutiwa katika orodha rasmi ya maandishi iliyorekodiwa katika Biblia ya Kanisa lenye madaraka lililokuwa likianzilishwa. Hata kama kanisa hilo halikuanzishwa na Yesu wa Nazareti, mwishoni mwa karne ya pili, kanisa

likaanza uchaguzi wa maandishi fulani. Ni mwisho wa karne ya 4 tu ndipo mchakato huo wa uteuzi wa maandishi ulifikia ukingoni.

Licha ya mageuzi iliyokithiri iliyofanyiwa maandiko ya Biblia, ukisoma maandiko hayo, utagundua mara tena mabaki ya imani kuhusu kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili na maisha ya awali ya nafsi kabla ya kuingia mwilini.

Ndani ya kitabu cha Hekima (8.19), mna aya wazi zinazozungumzia kuhusu maisha ya awali ya nafsi kabla ya kuingia mwilini. Suleimani, mwandishi wa sehemu hiyo ya Biblia, anasema yafuatayo kuhusu yeye mwenyewe: «*...Nilikuwa mtoto mwenye vipawa, nilipokea nafsi nzuri, au tuseme, kwa sababu nilikuwa nafsi adilifu, nikaingia katika mwili safi.*»

Agano Jipya pia linatoa maelekezo juu ya kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili. Kwa mfano, Yesu anaswali wanafunzi Wake: «Watu wanasema nini kuhusu Mwana wa mtu?» Wakamjibu, «*Wamoja husema wewe ni Yohana Mbatizaji, wengine husema wewe ni Eliya, na wengine tena husema wewe ni Yeremia au nabii mwingine.*» (Mt. 16:13-14) Wayahudi

ambao waliishi wakati wa Yesu walikuwa na uhakika kwamba mtu anaweza kuzaliwa upya mara kadhaa.

Uthibitisho wa Origene (185-254), ulionukuliwa hapo juu, unatuonyesha kwa kiwango gani mafundisho ya kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili ilikuwa inafundishwa kwa bidii katika Ukristo wa awali kabla ya kutupiliwa mbali kutokana na njama ya tabaka la makasisi. Bila shaka, Origene alikuwa mtu maarufu na mwana falsafa mkuu wa zama za kale za kikristo. Zaidi ya karne tatu, elimu yake na maisha yale viliangazia watu kiroho katika eneo lote la Mediterania. Kwa mfano, Maisha ya awali ya nafsi kabla ya kuingia mwilini, ilikuwa sehemu ya mafundisho ya Origene.

Hata hivyo aliishi, katika nyakati za mabadiliko ya Ukristo wa awali kuwa shirika lenye madaraka linalotegemea ibada ya nje na mila na desturi za kipagani. Tayari maishani mwake alishambuliwa vikali. Karibu mwisho wa karne ya ine.

Maandishi ya Origene yalibadilishwa na kuteketezwa na waakilishi wa Kanisa. Kwa sasa, hakuna kilichobaki cha maandishi asilia

ya Origene. Licha ya hayo, mafundisho yake yalitangazwa kwa kiwango kikuu sana, kupitia Arius (c. 260-336) na Wulfila (313-383), katika sehemu kubwa za Ulaya, mafundisho hayo yaliitwa «Arianismu». «Mafundisho potovu» hayo yalichukiza sana Kanisa. Kwa hivyo, wakati wa kongamano la mwaka 543 huko Konstantinople, Mfalme Justinia akapiga marufuku mafundisho ya Origene, au tuseme marufuku tisa kama ya kijeshi ikalenga sehemu za mafundisho zilizobaki na kujulikana bado wakati ule.

Laana hizo hazikutaja moja kwa moja kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili mpya, ila zikataja tu maisha ya awali ya nafsi kabla ya kuingia mwilini «marudio ya hali njema kwa vitu vyote», yaani, mafundisho inayosema kwamba wanadamu wote na nafsi zote watajumuika siku moja kando ya Mungu, na hivyo «laana ya milele» haikuwepo. Kwa njia hiyo, mafundisho ya kuzaliwa upya kwa nafsi duniani ya ukristo asilia ikanyamazishwa. Lakini kwa nini hivyo? Kwa sababu imani ya kuzaliwa upya kwa nafsi ndani ya mwili mpya, inakomboa wanadamu toka mafundisho na sheria zilizoanzishwa na Kanisa...

Jerome [mwandishi wa Biblia] angeliandika ndani ya Biblia sehemu za mafundisho ya ukristo asilia ya kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili iliyokuwa ndani ya maandishi ya Origene na ndani ya vitabu vya injili apokrifa tofauti, angelitangaza mafundisho hayo katika nchi za magharibi, bila shaka miaka 1700 iliyopita ingelikuwa ya heri sana.

Dunia ingeliishi kila siku katika heshima ya maadili safi, kwa sababu ufahamu wa jukumu la kila mmoja kuhusu maisha na tabia yake mwenyewe hutokana na ufahamu wa kuzaliwa upya kwa nafsi ndani ya mwili mpya na wa kanuni ya panda na vuna.

Ila, badala ya kufundisha kuzaliwa upya kwa nafsi duniani na upendo wa Mungu kwa wanae, badala ya kufundisha kwamba Mungu hukaa ndani ya kila mmoja wetu, kwamba Yeye ni Uzima ndani ya kila kitu na kwamba dunia ni mahali ambapo nafsi zote zilizopotoka zinaweza kujirekebisha – kama jinsi Yesu, Kristo, alivyofundisha mitume wake na hata pia sisi – Kanisa likafundisha mafundisho ya nje inayotawaliwa na ibada iliyo na msingi wa dhabihu ya umwagaji damu kama ya zama ya

watu wa maweni, na likafundisha pia hukumu wa milele uliotiwa na Mungu katili.



Lakini wakati umefika ambapo Kristo wa Mungu, kupitia unabii uliotolewa na Gabriele, nabii-mwalimu na mjumbe wa Mungu kwa wakati wetu huu, anafafanulia mara tena walimwengu ujuzi wa kuzaliwa upya kwa nafsi katika mwili mpya. Zaidi ya miongo mine sasa, kama jinsi Yesu alivyosema kupitia unabii, imepita sasa miaka 2000, Mungu, Mwenyezi, Baba, katika wema wake mkuu, anasema tena na wanae na kutuongoza katika ukweli wote, kwa kiwango ambacho wanadamu wanaweza kuufahamu ukweli huo...



Mwanadamu huvuna kile alichokipanda. Mambo yanayotupata katika uzima huu ni sisi wenyewe ndio tuliyasababisha, katika maisha yetu mengine ya awali. Leo, kwa msaada wa Kristo wa Mungu, tuna uwezo wa kutambua na kurekebisha sababu ya mambo inayotupata. Je, hiyo si neema kubwa? Tunaweza kumshukuru Mungu kwamba anaendelea kutupa bahati mpya ya kujiweka huru toka dhambi na kujitakasa – kinyume na madai ya Kanisa isemayo kwamba tuna uzima mmoja tu ambamo vyote hutolewa uamzi mara moja tu.

Marudio ya nafsi katika mwili mpya hayana uhusiano na tendo la «kujikomboa mwenyewe» kwa nafsi, ambalo linafuta umuhimu wa tendo la ukombozi wa Mnazareti. Bali, marudio ya nafsi katika mwili mpya ni nguvu ya ukombozi wa Kristo wa Mungu unaotuwezesha kusimama tena wakati tunapoanguka na kumrudilia Kristo mioyoni mwetu, inanatuwezesha tena kuendelea kujirekebisha zaidi kwa kutenda mapenzi yake...



Hapo awali, nafsi ilikuwa kiumbe safi cha kiroho katika Ufalme wa Mungu. Hata hivyo, viumbe vimoja vya kiroho vikamuasi Mungu, vikaanguka na, vikaanguka shimoni. Viumbe hivyo vilipenda kuwa mahali pote, kama jinsi Mungu alivyo, na kwa sababu hiyo vikapingana Naye, upinzani huo ndio ulisababisha anguko lao. Lakini kuona kwamba kuna Mungu mmoja tu, na Sheria moja tu kamilifu inayojumuisha vitu vyote, haiwezekani kwa kweli kupingana na Mungu. Yeyote anayefanya hivyo hupatwa na madhara ya kile anachosababisha mwenyewe, anavuna kile alichokipanda.

Hivyo ndivyo wakati wa maanguko, viumbe vilivyoanguka vilizidi kuchukua uzito zaidi na kubadilika toka muundo wa kiroho usio na uzito na kugeuka mwili ulio na maada nzito. Nafsi iliyo ndani ya vazi hilo la kimaada,au mwili, kama vile mwanadamu,inafuata kanuni ya panda na vuna ambayo nafsi iliunda yenyewe. Muda wote ambapo nafsi itategemea kanuni hiyo, itaibidi pia irekebishe machafuko iliyosababisha ndani ya mpango wa mambo ya ulimwengu kutokana na makosa yake. Jambo hilo ni lenye mantiki na ni sahihi.

Kuona kwamba Mungu aliwapa uhuru wanae, hatupashwi kusubiri, kama wanavyoshauri wana teolojia kwamba Mungu afute machafuko iliyosababishwa na mwenendo mbovu wa dhambi wa kila nafsi. Na uhuru huo unaohusiana na kanuni ya panda na vuna, unanipa wajibu wa kurekebisha madhara niliyosababisha mimi mwenyewe.

Tendo la Mungu kufuta dhambi zetu lina faida ipi? Ikiwa kwa mfano anamgeuza mtu mjeuri kuwa mpenda amani, yaani akimwondolea makosa na uovu aliowatendea wengine bila ya kuwa na dhamiri ya jambo hilo na kutubu na kubadilika,ni nini itakayojiri basi? Bila dhamiri, mtu huyo hatabadilika kamwe, baada ya muda kitambo atarudilia mambo hayo hayo, kwa mfano atarudilia ujeuri wake. Na ikiwa Mungu, kwa nguvu yake, akimshikilia mtu huyo katika tabia yake ya kupenda amani, je! mwanadamu huyo hatabaki kuwa kama kidude cha kuchezesha?...

Kila mwanadamu huchagua kuzaliwa upya kwa nafsi yake duniani au kufuata kwa dhati njia ya kurudi maskani kwa Baba. Ndiyo sababu Wamilele alifundisha Amri kumi kupitia Musa, tena ndiyo sababu Mwanae, Yesu, Kristo,

alikuja na akatufundisha upendo wa Mungu na njia ya kurudi kwa Baba. Kupitia upendo wake usio na mwisho kwetu sisi Wanadamu, Mungu alituletea uhuru na nuru.



Tukiishi kwa mujibu wa Amri za Mungu na mafundisho ya Yesu, Kristo, hatutakuwa tena na haja ya kurudilia maisha ya duniani baada ya kifo.

Turudilie jambo hili: Si mapenzi ya Mungu kwamba nafsi irudi kuishi duniani mara nyingi baada ya kifo. Kinyume na hayo, mapenzi yake ni kwamba, mwanadamu, muda huu wa maisha yake hapa duniani atakase nafsi na mwili wake kiasi kwamba uzima mpya duniani baada ya kifo usiwe na umuhimu tena kwake.

Duniani hatukutani na watu kwa kubahatisha. Inawezekana tukutane na watu kwa sasa kwa ajili ya kurekebisha hali fulani ya maisha yetu ya awali duniani. Vipi? Kwa kuwapa umuhimu watu ambao tunakutana nao, kwa kuwasikiliza na kabla ya yote kwa kusameheana.

Tukizingatia kwamba yanayotupata maishani yana sababu zake kwa sehemu kubwa katika maisha yetu ya awali kabla ya uzima huu, tutakuwa na mtazamo mzuri kuhusu Mungu. Hatutamshtaki tena haraka Mungu kuwa chanzo cha mambo maovu yanayotupata, bali tutafikia kujiswali kwamba hatima yetu haina uhusiano na nguvu mbovu tulizozitoa hapo awali na ambazo sasa zinatushambulia.

Hayo hayana maana kwamba tuna uwezo wa kufafanua na kubaini balaa inayowapata majirani wetu kwa sababu wao wenyewe ni wakosaji waajibikaji wa yale yanayowapata. Tukiwalaumu wengine kuhusu yanayotupata, tunajitia dosari ya dhambi, japo hakuna ajuaye matukio ya siku zijazo za maisha yake.

Kukubali hatima ya mtu binafsi, yaani kutowaajibisha wengine hakumaanishi kukubali hivyo hivyo na kumuachia wajibu wote! Hatima ya mtu haikuandikwa jiweni. Uzima si jambo lisilobadilika. Mungu anahitaji tushike Amri zake, Sheria yake kusudi tuwe salama. Tukimgeukia na tukijitahidi siku zote kuishi kwa mjibu wa Amri zake, inawezekana hatima yetu ichukue mwelekeo mzuri, ikiwa hayo ni vema kwa nafsi yetu.

Mara na mara tunasikia watu wakisema «kwa nini Mungu haingilii kati mambo hayo?» Mungu alitutolea uamzi huru, na kwa nini aingilie kati mapenzi yetu ya kiutu mno, kiburi chetu, ukatili wetu, matendo yetu iliyo kinyume na Amri zake?

Tukitazama mwendo wa matukio makubwa ya ulimwengu, tutatambua kwamba kwa namna fulani Mungu ameingilia kati mambo. Hakuingilia kati kanuni ya sababu na matokeo yake. Ila alitutumia mwana wake, kwa ajili ya kutuletea wokovu. Wokovu ni nini? Wokovu ni nuru iliyotiwa ndani ya nafsi kwa ajili ya ulinzi wake, kusudi isizame chini sana siku zote na kuharibika ndani ya cheche ya nuru kama hayo yanayofundishwa na dini za nchi za mashariki.



Ikiwa Kristo alituletea wokovu, ni vipi hukumu wa milele unaweza kuwepo? Hayo yanaonyesha hitilafu za wanatheolojia wanaohakikisha eti kupitia tendo la wokovu, Kristo alitukomboa toka dhambi zote. Ila, ikiwa nafsi zote zilikombolewa kwa gafla baada ya Yesu kutamka «Yote yamekwisha», ikiwa nafsi hizo hazina tena makosa, kwa nini dunia hii inazama sana ndani ya ubaya, matengano, vita, mauwaji na uadui? Hivyo vyote ni dhambi. Hivyo tunaona kwamba, Yesu, Kristo, hakufuta dhambi, kama jinsi kanisa inavyohakikisha na kwamba kinyume cha jambo hilo ndio ukweli. Kristo aliletea nafsi zote msaada wa nguvu na Yumo ndani mwetu kama nuru na nguvu, kama msaada unaomwezesha kila mmoja kujitakasa na hatimaye kurudi katika nchi ya milele, kama kiumbe safi cha kiroho.



Nafsi inapogeuka yenye nuru sana na ikiwa haina haja tena ya kurudilia maisha ya dunia, inaweza kujitakasa na kuendelesha mwendo wake katika mazingira ya utakaso iliyotajarishwa kwa kupokea nafsi katika ahera kwa ajili ya kukaribia sana nyumba ya Baba, kukaribia Uzima asilia wa milele. kukaribia nchi yake asilia.

Tutarudi sote kwa Baba ambako tulikotoka kwani ndani ya kila mmoja wetu mna kiumbe chenye nuru. Ni kiumbe hicho ndicho kinarudi nyumbani kwa Baba. Hakika Mungu hakuumba nafsi bali kiumbe cha nuru kilicho ndani mwake, kiumbe hicho kikijitakasa kinaonyesha nuru yake.

Kila mmoja wetu ni hekalu la Mungu, Mungu anaishi ndani mwetu. Jinsi tunavyoendelea kutimiza Amri zake na mafundisho ya Yesu, Kristo, ndivyo tunaendelea kumkaribia Baba Yetu wa Mbinguni na kupiga hatua tukitekeleza Amri, tukishika mkono wa Mwokozi wetu, kwa ajili ya kutoka kwenye marudio ya maisha baada ya kifo na kuingia katika Ufalme wa nuru, ndani ya Mungu, Yeye aliyetutazama na kutuumba ili tuishi milele.

Kwetu sisi wanadamu, ni faraja hakika kutambua kwamba baada ya uzima huu wa duniani, nafsi yetu inaweza kushika njia ielekeayo nchini kwake,ikiwa tulitekeleza Amri na Sheria za Mungu. Tayari Kristo alitutaarifu kuhusu nchi hiyo kupitia maneno haya:

«*Nyumbani mwa Babangu mna makao mengi, isingelikuwa hivyo ningewaambia kwamba ninaenda kuwaandalia makao? Na baada ya kwenda kuwaandalia makao, nitarudi kuwatwaa kusudi muwe nanyi mahali nilipo.*» (Yohana 14,2-3)

Makazi ya nchi hiyo na familia za kiroho zinangoja ujio wetu, Zinatukumbuka, zina kumbukumbu ya umoja mkuu wa ulimwenguni pote katika nyumba ya Baba. Na Nyumba ya Baba, ni Ufalme wa Mungu ulio na upeo usio na mwisho! Nguvu ya Mungu inamulikia upande wetu, ndiyo sababu manabii waliendelea kuja kuwahimiza wanadamu kwa maneno haya: «*Acheni uovu, mgeukieni Mungu, Mungu ni upendo. Baba anawapenda. Anapenda wana aliowaumba!*»

Mungu angekuwa katili sana ikiwa angetuadhibu na kutuwekea hukumu wa milele! Lakini hatendi hivyo. Yeye ni Baba

yetu na anatupenda. Jinsi tutakavyotakasa nafsi yetu, ndivyo tutakavyoenda kwa urahisi wakati saa yetu ya mwisho itakapokuja, kwani tutahisi kwamba Kristo ametushika mkono na anatuongoza hatua kwa hatua kuelekea maskani kwa Baba yetu. Hivyo marudio ya maisha ya duniani baada ya kifo yatakoma. Tutarudi moja kwa moja katika Ufalme wa Mungu!



Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
Gabriele-publishing.com

Vijitabu vitolewavyo bila malipo





Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake. *(Kurasa 48)*



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi huhitaji mafunzo, kwa kuwa sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu. *(Kurasa 56)*



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote. *(Kurasa 44)*



Roho huru – Mungu ndani mwetu

Kitabu kinamwelekeza msomaji kwenye njia ya uhuru na kinamuwezesha kujitenga na imani potovu, mila ngumu na taasisi zinazotushikilia. Njia hiyo ni njia iongozayo kwa Mungu, kwa Mungu ndani mwetu.
(Kurasa 76)



Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com